Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | July-2025

EAJK

# Uhawilishaji Mkazo wa Kiswahili kwa wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya Pili: Uchunguzi kifani wa wajifunzaji Warundi nchini Burundi

**Authors**

**Révocat Ndayizeye[1]; Michael Mashauri[2]**

**Main author's email: ndayizeyerevocat1991@gmail.com**

**(1.2) University of Dar Es Salaam, Tanzania**

**Cite this article in APA**

Ndayizeye, R., & Mashauri, M. (2025). Uhawilishaji mkazo wa Kiswahili kwa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili: Uchunguzi kifani wa wajifunzaji Warundi nchini Burundi. *Eastern Africa journal of kiswahili,* 4(1), 39-54. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.759

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-05-14
Accepted: 2025-06-13
Published: 2025-07-14

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright:** ©2025 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.

**Ikisiri**

Makala hii imechunguza uhawilishaji mkazo wa Kiswahili kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza lugha hiyo kama lugha ya pili. Lengo kuu la makala hii ni kuchunguza namna mkazo unahama kutoka silabi moja hadi nyingine kwenye maneno yaliyodhihirisha uhawilishaji mkazo kwa wajifunzaji. Data zilikusanywa kutoka kwa wajifunzaji wa Kiswahili vyuo vikuu viwili vya serikali nchini Burundi. Sampuli ya utafiti ni wanafunzi 20, 10 kutoka Chuo Kikuu cha Ualimu cha Burundi na 10 kutoka Chuo Kikuu cha Burundi. Sampuli hiyo ya wanafunzi ishirini iliteuliwa kuanzia dawati la kwanza hadi la mwisho huku akiruka dawati moja moja. Alifanya hivyo kwa kila darasa. Baada ya kumaliza kazi hiyo ya kuchagua wanafunzi mtafiti aliomba waliochaguliwa kusimulia hadithi wanazojua mmoja hadi mwingine huku akirekodi masimulizi kwa ajili ya uchambuzi wa baadaye. Ili kufikia lengo la makala hii watafiti walitumia mbinu ya masimulizi ya hadithi. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Mizani ambacho ni kiunzi cha nadharia kilichopendekezwa na Liberman (1977) baadaye kikaendelezwa na Liberman na Prince (1977) na Halle na Vergnaud (1978). Watafiti walitumia pia programu ya "Praat" katika kuonesha namna nguvumsikiko ulivyokuwa katika kila kiambajengo. Vilevile, watafiti wametumia matawi katika kuonesha utofauti wa gridi kwenye silabi zinazounda neno. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa Warundi huhamisha mkazo kutoka silabi ya mwisho kasoro moja kwenda katika silabi nyingine tofauti katika maneno teule. Kadhalika, makala hii imependekeza kwa tafiti fuatizi yafuatayo: utafiti mwingine ufanyike katika vyuo vikuu vilivyoko mikoani ili kuona kuwa hali kama hiyo ipo. Aidha, utafiti mwingine uchunguze kiimbo, kidatu, au lafudhi tofauti na mkazo. Isitoshe, utafiti ufanyike ili kuchunguza mbinu zinazotumika kufundishia lugha hiyo ya Kiswahili kama zinafaa au la.

**Maneno muhimu:** Kiambajengo, lugha, mkazo, silabi, uhawilishaji.

## UTANGULIZI

Nchini Burundi Kiswahili ni lugha inayofundishwa kama lugha ya pili kuanzia shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Kwa utafiti wa awali uliofanyika, unaonesha kuwa Wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili vyuoni wanapotamka baadhi ya maneno ya Kiswahili wanahawilisha mkazo. Aidha, kuhawilisha mkazo kutoka kwenye silabi moja hadi nyingine kunasababisha utamkaji usio sahihi wa maneno ya Kiswahili wanayojifunza. Jambo lililochochea watafiti kufanya utafiti huu.

Katika taaluma ya isimu matumizi, uhawilishaji ni mchakato wa uhamishaji wa mawazo yaliyo katika maandishi au mazungumzo kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa njia ya maandishi au mazungumzo (Newmark, 1983). Katika makala hii tumetumia uhawilishaji kumanisha uhamishaji wa mkazo kutoka silabi moja kwenda silabi nyingine katika maneno teule. Dhana ya mkazo imefasiliwa na watalaamu mbalimbali wakiwamo Hogg na MchCully (1987) wanaodai kuwa mkazo ni kipandesauti huru cha irabu ambacho kinawakilishwa na seti za sheria. Hata hivyo, Massamba (2004) anaeleza kuwa mkazo ni hali ya neno au silabi katika neno kusikika kuwa na nguvu zaidi kuliko maneno au silabi nyingine. Fasili hiyo inaendana na ya Kihore, Massamba na Msanjila (2008) ambao wanaeleza kuwa mkazo ni utaratibu wa utamkaji wa maneno ambapo silabi fulani hutamkwa kwa nguvu nyingi zaidi kuliko ilivyo katika silabi nyingine za neno hilohilo. Kwa upande wa Crystal (2008) mkazo ni kiwango cha nguvu kinachotumiwa kutamka silabi, nguvu hiyo huweza kutofautisha silabi zenye mkazo wenye nguvu ambazo hutamkwa kwa nguvu zaidi na silabi zenye mkazo hafifu ambazo hazitamkwi kwa nguvu sana.

Kutokana na fasili zote hizo, katika utafiti wetu tumejikita katika fasili ya Crystal (2008) kwa maana fasili hii inaonesha kuwa mkazo ni hali ya silabi moja kuwa na nguvumsikiko mkubwa zaidi kuliko nyinginezo zinazounda viambajengo vya neno husika. Aidha, kwa mantiki hiyo hiyo, msikiko wa nguvu hiyo unatofautiana kutoka silabi moja hadi nyingine. Hii ina maana kuwa baadhi ya silabi huwa na nguvumsikiko zaidi kuliko nyingine. Pia, zimepewa alama N katika kazi hii ilihali silabi ambazo zina msikiko ambao ni hafifu zimepewa alama ya H.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Lugha ya Kiswahili kama lugha nyinginezo za Kibantu ni lugha yenye mkazo (Ashton, 1944). Ina maana kuwa Kiswahili ni lugha ambayo katika kuitamka mkazo unajitokeza tofauti na lugha nyingine za kigeni kama Kiingereza. Aidha, katika lugha ya Kiswahili mkazo huwa unajitokeza katika silabi ya mwisho kasoro moja katika neno. Kwa mujibu wa Ashton (1944), kuna maneno yaliyo machache yaliyokopwa kutoka lugha ya kiarabu ila hayo maneno yana mkazo katika silabi ya kwanza mwa neno. Naye Polome (1976) anaeleza kuwa mkazo katika lugha ya Kiswahili unajitokeza katika silabi ya mwisho kasoro moja katika neno.

Kuhusiana na maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kiarabu mkazo unajitokeza katika silabi ya kwanza ya neno. Pembeni na maelezo yake kuhusu mkazo katika Kiswahili, Polome (1976) anaenda mbali kwa kuhusisha mkazo na fonimu. Anasema kuwa mkazo una sifa za fonimu. Ila maelezo ya mtaalamu Mwansoko (1995) anaeleza kuwa Vital (1985) alikosoa mgongano huu. Hivyo, alithibitisha kuwa yanaelekea wazi mkazo katika Kiswahili hauna sifa za fonimu. Hata hivyo, wajifunzaji Warundi wanaojifunza lugha ya pili huwa wanahawilisha mkazo kutoka silabi moja hadi nyingine, kama anavyodai Gélase (2013) kuwa wajifunzaji Warundi wanapoongea Kifaransa ,huwa wanahamisha mkazo kutoka silabi moja kwenye neno hadi nyingine. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyodhihirika kuhamishiwa mkazo kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Masuba (2013) alifanya utafiti katika lugha ya Kinyakyusa na kuchunguza iwapo lugha hiyo ina toni au mkazo ama vyote pamoja. Mtaalamu huyu alibaini kuwa lugha ya Kinyakyusa licha ya kuwa na viinitoni katika baadhi ya misamiati kuna udhihirikaji wa mkazo katika baadhi ya misamiati yake. Aidha, aliweza kubainisha msigano wa nguvumsikiko unavyojitokeza katika lugha hiyo. Masuba (2013) aligundua kuwa utokeaji wa mkazo huweza kutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Hivyo, katika utafiti wa sasa, mtafiti ataangalia ujitokeaji wa mkazo katika lugha ya Kiswahili kwa wajifunzaji Warundi ambao lugha yao ni Kirundi ambayo mkazo unaweza kuwa tofauti na Kiswahili. Hili litatazamwa kwa makini ili kuja na hitimisho kuwa wanahawilisha mkazo kwa Kiswahili

kutokana na sababu tutakazopata kutoka kwa washiriki uwandani.

Pia, Gélase (2013) alifanya utafiti kuhusu mkazo katika lugha ya Kifaransa kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza lugha hiyo. Mtafiti huyo alibainisha kuwa wajifunzaji hao wanahawilisha mkazo kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hata hivyo, mtafiti wa sasa hatashughulika na lugha hiyo ya Kifaransa ila ataangalia ikiwa wajifunzaji Warundi wanapojifunza Kiswahili wanahamisha mkazo au la.

Mgullu (1999) na Massamba et al. (2004) wanaeleza kuwa lugha za Kibantu zenye mkazo zina mkazo ambao ni funge kwa maana kuwa mkazo wenyewe huangukia katika silabi maalumu ya neno, uhalisia ni kwamba hali inaweza kuwa tofauti kwa baadhi ya lugha kama vile Kinyakyusa. Halle na Clements (1983) wanasema kuwa kuna utofauti ya uwekaji mkazo kati ya lugha moja na nyingine. Kwa mfano wanasema kuwa katika lugha ya Kimaranguku, mkazo msingi unawekwa katika silabi ya kwanza ya neno lakini lugha ya Kiweri, mkazo msingi unawekwa katika silabi ya mwisho. Hivyo, kutokana na utofauti huo, mtafiti wa sasa alichunguza iwapo wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Warundi wanahamisha mkazo wanapotamka baadhi ya maneno ya Kiswahili.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Mizani (NFM) iliyoasisiwa na Liberman (1977) kama kiunzi cha kinadharia na kuendeleza na Liberamn na Prince (1977) na Halle na Vergnaud (1978). NFM ina mihimili mitatu lakini katika kazi hii tulitumia tu mhimili mmoja tu wa tatu ambao ni uhusiano wiani wa matawi. Watafiti walitumia mhimili huu kwa kuwa unaonesha msigano wa nguvumsikiko katika viambajengo vinavyohusika ambapo matawi hayo hudhihirisha msigano huo wa nguvumsikiko Hii hujidhihirika pale ambapo huwa na uwiani wa kimsikiko. Hivyo, katika mhimili huu tawi moja huwa na msikiko zaidi kuliko tawi jingine. Tawi lenye msikiko zaidi huwa na nguvu zaidi na katika uchanganuzi lilipewa alama ya **N.** Alama hii inafasiliwa na kusomeka kama ina nguvu zaidi kuliko matawi mengine au silabi nyingine katika viambajengo vinavyounda neno husika, wakati lile lisilo na msikiko zaidi huwa hafifu na katika uchanganuzi lilipewa alama ya **H.** Alama hii hufasilika na kusomeka kama hafifu kuliko matawi mengineyo au silabi nyinginezo (Liberman & Prince, 1977).

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti ulifanyika katika vyuo vikuu viwili vya serikali nchini Burundi. Sampuli ya utafiti huu ni wanafunzi ishirini (20), kumi (10) kutoka Chuo Kikuu cha Ualimu cha Burundi na kumi (10) kutoka Chuo Kikuu cha Burundi. Usampulishaji nasibu sahili ndio ulitumika katika kuteua sampuli ya wanafunzi ishirini kwa kuwa kila mtoa taarifa alikuwa ana haki sawa na mwingine. Sampuli hiyo ya wanafunzi ishirini iliteuliwa kuanzia dawati la kwanza hadi la mwisho huku akiruka dawati moja moja. Alifanya hivyo kwa kila darasa. Baada ya kumaliza kazi hiyo ya kuchagua wanafunzi mtafiti aliomba waliochaguliwa kusimulia hadithi wanazojua mmoja hadi mwingine huku akirekodi masimulizi kwa ajili ya uchambuzi wa baadaye.

Wanafunzi ishirini walihusishwa katika makala hii kwa kuwa mtafiti aliona kwa matumizi ya mbinu ya masimulizi ya hadithi data zinapatikana zikiwa nyingi haraka. Aidha, katika utafiti huu tulitumia mbinu ya masimulizi ya hadithi ili kupata data za kifonolojia. Vilevile, kinasasauti kilitumika kurekodi data kutoka kwa watoataarifa. Kadhalika, ili kuonesha namna silabi zinatofautiana matamshi yake, tulitumia matawi ya fonolojia mizani ili kuonehsa gridi katika kila viambajengo vya maneno teule. Isitoshe, katika uchambuzi data programu ya *Praat* ilitumika ili kuonesha nguvumsikiko wa viambajengo vilivyounda maneno teule. Mtafiti alipeleka maombi ya kibali katika Chuo Kikuu cha Ualimu pamoja na Chuo Kikuu cha Burundi ambapo pia alipewa vibali vya kuonana na watoataarifa. Mtafiti alipokuwa uwandani alijitambulisha na kueleza lengo la utafiti, hali hiyo iliwasaidia watoataarifa kumfahamu na kumpa ushirikiano zaidi. Pia, mtafiti aliwahakikishia kuwa taarifa zilizotolewa zitakuwa ni siri.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Katika sehemu hii, mtafiti alizungumzia maneno ambayo yamedhihirika kwa watoataarifa kuhawilisha mkazo wakati walikuwa wanasimulia hadithi darasani, wakati wa ukusanyaji wa data. Makala hii ilibainisha aina nne za maneno kudhihirika kuhawilisha mkazo kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Makala ilianzia nomino kisha na kufuatisha aina nyinginezo.


**Nomino Zilizodhihirisha kuhawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji**

Baada ya kubainisha maneno yote yaliyohamisha mkazo na kuyaweka katika jedwali kwa kuzingatia aina yake, mtafiti alishughulikia suala la kuonesha nguvumsikiko unavyojibainisha katika silabi zinazounda neno linalohusika ili kuweza kubaini utokeaji wa mkazo katika silabi zinazounda neno hilo.

**Jedwali 1: Nomino zilizohawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji wa Kiswahili**


| No | Nomino zilizohawilisha mkazo | Nomino namna zinatakiwa kuwekewa mkazo |
|---|---|---|
| 1 | Kijana: /ˈKiɟana/ | Kijana: /Kiˈɟa:na/ |
| 2 | Sahani:/ˈsahani/ | Sahani:/saˈhani/ |
| 3 | Kirundo:/ˈkiru:ndɔ/ | Kirundo:/ˈkiru:ndɔ/ |
| 4 | Masomo:/ˈmasɔmɔ/ | Masomo:/maˈsɔmɔ/ |
| 5 | Kipaji:/ˈKipaɟi/ | Kipaji:/Kiˈpa: ɟi/ |
| 6 | Kipato:/ˈkipatɔ/ | Kipato:/kiˈpatɔ/ |
| 7 | Mwanafunzi:/ˈmwanafu:nzi/ | Mwanafunzi:/mwanaˈfunzi/ |
| 8 | Mchakato:/ mtʃa:ˈkatɔ / | Mchakato:/ mtʃaˈkato / |
| 9 | Mzalendo:/ˈmza: lɛndɔ / | Mzalendo:/mzaˈlɛndɔ / |
| 10 | Bubanza:/ˈbuba:nza / | Bubanza:/buˈbanza / |
| 11 | Mchumba:/ˈmʧu:mba/ | Mchumba:/mˈʧumba/ |
| 12 | Asubuhi: /a:ˈsubuhi/ | Asubuhi: /a:suˈbu:hi/ |
| 13 | Wazo:/ˈwa:zɔ/ | Wazo:/ˈwazɔ/ |
| 14 | Binti: /ˈbi:nti/ | Binti: /ˈbinti/ |
| 15 | Hadithi: /ha:di:θi/ | Hadithi: /haˈdi:θi/ |
| 16 | Jina:/ˈɉi:naˈ/ | Jina:/ˈɉi:na/ |
| 17 | Muramvya:/mˈra: vja / | Muramvya:/mraˈvja / |
| 18 | Gisangana: /giˈsa: ŋgana/ | Gisangana: /gisaˈŋgana/ |
| 19 | Maji:/ma:ɟi/ | Maji:/ˈma:ɟi/ |
| 20 | Nyama:/ɲamaˈ/ | Nyama:/ˈɲama/ |
| 21 | Kuni:/ku:niˈ/ | Kuni:/ˈku:ni/ |
| 22 | Mvulana:/ˈɱvula:na/ | Mvulana:/ɱvuˈla:na/ |
| 23 | Shoka:/ʃɔ:kaˈ/ | Shoka:/ˈʃɔ:ka/ |
| 24 | Panya:/paɲaˈ/ | Panya:/ˈpaɲa/ |
| 25 | Kinyonga:/ˈkiɲɔ:ŋga/ | Kinyonga:/kiˈɲɔŋga/ |

Kama ilivyobainishwa katika jedwali na.hapo juu ni kuwa wajifunzaji wamehamisha mkazo msingi kwenye hizo nomino hamsini (50). Hayo yamedhihirika baada ya kusikiliza mara kadhaa rekodi zilizopatikana kutoka uwandani. Aidha, kama kazi yetu inavyotakiwa kutumia NFM, tulianza kwanza kuchambua baadhi ya nomino kinadharia ili kuonesha hali ya msikiko katika viambajengo vinavyounda maneno husika. Isitoshe, ili kuonesha bayana namna mkazo msingi unavyojibainisha kwenye baadhi ya viambajengo tulivyonavyo, programu ya ***"PRAAT"*** imetumika kwa kutuwezesha na kuthibitisha kile kilichokwishaoneshwa kupitia matawi ya NFM. Tazama mfano Na.1: **Kijana: /Kiˈɉa:na/** lilotamkwa kama **Kijana: «ˈKiɟana'»** kutoka kwa watoataarifa.




Uchanganuzi wa data katika mfano Na.1 unaonesha namna msigano wa nguvumsikiko wa mkazo unavyojibainisha katika neno hilo katika umbo lake la ndani. Hivyo, kimsikiko silabi ya mwisho kasoro moja ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi ya mwisho ya neno hilo. Aidha, kutokana na msigano wa kimsikiko silabi /**ja**/ ndiyo inayosikika kwa nguvu zaidi inapewa alama **N** kuonesha kuwa ina nguvu zaidi kimsikiko kuliko silabi iliyobaki ambayo imepewa alama H huonesha kuwa silabi hiyo ina msikiko hafifu zaidi tofauti na silabi ya mwisho kasoro moja ambayo katika neno hilo ni silabi ya kwanza na ya mwisho.


Kawaida neno kijana linatakiwa kuwa kama inavyoonekana kwenye kielelezo na.hapo juu. Hapa tunaona kuwa nguvumsikiko unajibainisha kwa silabi /ɟa/ kama inavyoonesha makadirio ya desibeli **39.00** kwenye kielelezo hapo juu.





**Kielelezo 1: Mkazo katika Silabi za neno «ki'jana» (matamshi sahihi)**

Watalaam wakiwamo Polomé (1967), Mgullu (1999), Massamba et al. (2004), Massamba (2004), Massamba (2011), Massamba (2012) na Kindija (2012) kwamba katika Kiswahili mkazo msingi katika kiwango cha neno huwekwa katika silabi ya mwisho kasoro moja. Ni kwa mantiki ya hoja hii kuwa neno ***kijana*** tuliweza

kuliwakilisha katika kielelezo hicho na baadaye tuje kuonesha matokeo ya matamshi ya neno hilo hilo kwa wajifunzaji wetu wa Kiswahili vyuo vikuu vya serikali Burundi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili nchini huo. Tazama kielelezo Na.2 Hapo chini.




Uchaganuzi wa mfano Na.2 unaonesha namna msigano wa nguvumsikiko unavyojitokeza kwenye neno hilo katika umbo lake la ndani. Inaonesha silabi ya kwanza ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine katika neno hilo. Silabi **/ki/** ndiyo inaonesha alama **N** kuonesha kuwa ina nguvu zaidi kimsikiko kuliko silabi zilizobaki.Hii ina maana kuwa wajifunzaji Warundi wamehamisha mkazo kutoka silabi **/ja/** ya mwisho kasoro moja na kuweka mkazo kwenye silabi ya kwanza **/ki/** katika neno hili ***kijana.***




**Kielelezo 2: Mkazo katika Silabi za neno «'kijana» (matamshi yasiyo sahihi)**

Ni shahiri dhahiri kuwa utafiti wetu si wa kulinganisha ila kwa kuwa tulishughulikia matamshi ya Kiswahili kwa wajifunzaji, mtafiti ameona ahusishe matamshi sahihi na yale yaliyodhihirisha uhamishaji mkazo ili kurahisishia msomaji kuelewa haraka zaidi. Hivyo, kama ilivyoonekana kwenye kielelezo hicho hapo juu, tunaona matamshi ya nomino ***kijana*** kwa wanafunzi Warundi yameonesha kuwa makadirio ya silabi **/ki/** yameonekana kuwa na makadirio ya desibeli **38.00.** Silabi nyingine zimeonekana hafifu zaidi kuliko silabi hiyo.

**Vitenzi vilivyodhihirisha kuhawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji**

Sehemu hii makala ilizungumzia vitenzi vilivyodhihirika kuhawilisha mkazo kwa wajifunzaji Warundi. Tazama






Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

aya zinazofuata. Kama jedwali Na.2 linavyobainisha uwezekano wa vitenzi kadhaa kudhihirisha uhamishaji wa mkazo hasa mkazo msingi kwenye silabi zinazounda vitenzi hivyo, mtafiti baada ya kubainisha vitenzi hivyo alionesha kwa baadhi ya vitenzi teule nguvumsikiko kwa viambajengo hapa chini.


**Jedwali 2: Vitenzi vilivyohawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji Warundi**

| No | **Vitenzi vilivyohawilisha mkazo** | **Uwakilishi kifonetiki usio sahihi** | **Uwakilishi kifonetiki wenye mkazo sahihi** |
|---|---|---|---|
| 1 | Alipoona magari hajamsogelea | /aˈlipɔɔna magari haˈjaɟamsɔgɛlɛja/ | Alipɔˈɔna magari hajaɟamsɔgɛˈlɛja/ |
| 2 | Akaaga duni | /aˈkaaga duˈnija/ | /akaˈaga duˈnija/ |
| 3 | Hajanitega sikio | /haˈʄanitɛga siˈkijɔ/ | /haɟaniˈtɛga siˈkijɔ/ |
| 4 | Kinachosikitisha | /kiˈnaʧɔ:sikitiʃa/ | /kinaʧɔ:sikiˈtiʃa/ |
| 5 | Walichoweza kufanya | /waˈliʧɔwɛ:za………/ | /waliʧɔˈwɛ:za………/ |
| 6 | Alimkatalia katakata | /alimka:taalia ˈkataˈkata/ | /alimka:taalia kataˈkata/ |
| 7 | Anachotaka | /ana:ʧɔ:taka/ | /anaˈʧɔ:taka/ |
| 8 | Akafika sokoni | /aka:fika sɔ:kɔni/ | /akaˈfika ˈsɔkɔni/ |
| 9 | Alipokuwa karibu | /alipo:kuwa karibuˈ/ | /alipoˈkuwa karibu/ |
| 10 | Tumngojee | /ˈtumŋgɔ:ɟɛɛ/ | /tumˈŋgɔ:ɟɛɛ/ |
| 11 | Kutoka mkoani | /ˈkutɔka……/ | /kuˈtɔka……/ |
| 12 | Kuingia maisha mapya | /ˈkuiŋgija………./ | /kuiˈŋgija………./ |
| 13 | Anasoma | /anˈasɔma/ | /anaˈsɔma/ |
| 14 | Akahuzunika | /akahuzunika/ | /akahuzunika/ |
| 15 | Akaenda nyumbani kwake | /aˈkaɛnda…………../ | /akaˈɛnda…………../ |

Aidha, kama kazi yetu inavyotakiwa kutumia NFM, tulianza kwanza kuchambua baadhi ya nomino kinadharia ili kuonesha hali ya msikiko katika viambajengo vinavyounda maneno husika na baadaye matumizi ya programu ya Praat. Tazama mfano wa uchanganuzi wa kitenzi **akaaga** kwa kutumia matawi na baadaye matumizi ya programu ya *PRAAT*.




Uchanganuzi wa data katika mfano **Na.3** wa kitenzi **akaaga** unaonesha namna msigano wa nguvumsikiko wa mkazo unavyojibainisha katika neno hilo katika umbo la ndani. Katika mfano huu pia silabi ya mwisho kasoro moja **/a/** ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine zinazounda neno hilo. Hivyo, silabi inayosikika kwa nguvu zaidi inapewa **N** kuonesha kuwa ina nguvu zaidi kimsikiko kuliko silabi nyingine zinazounda neno hilo.




**Kielelezo 3 : Mkazo katika Silabi za neno «aka'enda» (matamshi sahihi)**


Kielelezo Na.3 kimeonesha msigano wa nguvumsikiko ambao umejibainisha katika kitenzi hicho hapo juu. Katika hali ya kawaida ya matamshi ya kitenzi chetu **"akaenda"** programu yetu **PRAAT** imetupa matokeo ya kuwa silabi yenye nguvumsikiko zaidi ni **/e/** ambayo ipo mwisho kasoro moja kama watalaam wanadai kuwa kawaida inatakiwa kuwa hapo hapo. Silabi hiyo imeonekana kwa katika kilele kifikapo **26.00.** Silabi nyinginezo zimeonekana hafifu ila uhafifu wake unatofautiana kutoka silabi moja hadi nyingine.




Mfano Na.3 unaonesha katika uchanganuzi wa mkazo namna msigano wa nguvumsikiko unavyojitokeza kwenye neno hilo katika umbo lake la ndani. Inaonekana kwenye tawi hilo kuwa silabi **/ka/** ndiyo ina

nguvu msikiko zaidi kuliko silabi nyingine. Hivyo, kutokana na msigano wa nguvu msikiko silabi inayosikika kwa nguvu zaidi inapewa alama **N** kuonesha kuwa ina nguvu zaidi kimsikiko kuliko silabi zilizobaki. Ila mfano Na.3 unaonesha wazi kuwa uchanganuzi ungeishia tu katika miti ya mizani. Viambajengo hivyo vinaonesha usawa kimsikiko kuna viambajengo vinavyotamkwa kwa nguvu zadi na vingine vinatamkwa hafifu. Hivyo, kwa kutumia gridi imewezesha kubainisha kwa uwazi kuwa silabi /ka/ ndiyo inatamkwa kwa nguvu zaidi kuliko silabi nyingine zinazounda neno hilo kwani imekuwa na gridi mbili ilihali nyingine zote zipo chini ya mbili.

Hapa tumeona kuwa wajifunzaji Warundi katika mchakato wa kujifunza Kiswahili ikiwa Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali Burundi wamehamsiha mkazo kabisa. Mathalani kwenye kitenzi hiki **akaaga,** imegundulika kuwa wamehamisha mkazo uliokuwa kwenye silabi ya mwisho kasoro moja na kuwekwa kwenye silabi ya pili kwenye neno hilo ambayo ni **/ka/.** Tazama Kielelezo Na.3 kinachothibitisha matamshi hayo ya neno hilohilo kama lilivyooneshwa kinadharia hapo juu kwenye mfano Na.3 .




**Kielelezo Na.4: Mkazo katika Silabi za neno «a'kaaga» (matamshi yasiyo sahihi)**

Kielelezo Na3. kinaonesha nguvumsikiko miongoni mwa silabi hizo ambazo zimeunda kitenzi ***akaenda***. Silabi **/a/ ya** mwanzo katika kitenzi hiki ndiyo ina nguvumsikiko kubwa zaidi ambayo katika kilele chake imefikia kiwango cha **24.00** ambayo ni kubwa kuliko silabi nyingine zote katika kitenzi hicho. Silabi **/ka/** inafuatia ambayo katika kilele chake inaonesha 20.00. Pia, silabi /**e**/ inafuatia ambayo katika kilele cha 4.00 na mwisho kabisa inasomeka silabi /**nda**/ ambayo kilele chake ni cha 0.00. Kwa mujibu wa matamshi sahihi silabi /e/ ingetakiwa kuwa na nguvumsikiko mkubwa kuliko nyingine ila haijawa kama hivyo. Kwa hiyo, wajifunzaji wamehawilisha mkazo katika matamshi yao.


**Vivumishi vilivyodhihirisha kuhawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji**

Sehemu hii makala ilizungumzia vivumishi vilivyodhihirika kuhawilisha mkazo kwa wajifunzaji Warundi. Tazama aya zinazofuata.


**Jedwali Na.3: Vivumishi kama Maneno yaliyodhihirisha Mkazo kwa Wajifunzaji**

| Na. | Vivumishi vilivyohawilisha mkazo | Uwakilishi kifonetiki usio sahihi | Uwakilishi kifonetiki wenye mkazo sahihi |
|---|---|---|---|
| 1 | mweusi | /mwɛ:usi/ | /mwɛ'usi/ |
| 2 | Kijana **mbaya** | /mbaja/ | /mba'ja/ |
| 3 | mmoja | /mmɔ:ɟa/ | /m'mɔ:ɟa/ |
| 4 | Wastani | /wa:stani/ | /was'tani/ |
| 5 | Kidogo | /ki'dɔgɔ/ | /ki'dɔ:gɔ/ |
| 6 | Wachache | /waʧa:ʧɛ/ | /wa'ʧa:ʧɛ/ |
| 7 | mkorofi | /m'kɔrɔ:fi/ | /mkɔ'rɔ:fi/ |
| 8 | kizungu | /'kizuŋgu/ | /ki'zuŋgu/ |
| 9 | kifalme | /'kifalmɛ/ | /ki'falmɛ/ |
| 10 | kitajiri | /kita: ɟiri/ | /ta:'ɟiri/ |
| 11 | mkali | /mka:li/ | /m'kali/ |
| 12 | Mombasa | /'mɔmbasa/ | /mɔm'basa/ |
| 13 | kiholela | /kihɔ:lɛla/ | /kihɔ:'lɛla/ |
| 14 | Ovyoovyo | /ɔvjɔ:ɔvjɔ/ | /ɔvjɔ'ɔvjɔ/ |
| 15 | kiungwana | /kiju:ŋgwa'na/ | /kiju'ŋgwa:na/ |

Kama jedwali Na.3 linavyobainisha uwezekano wa vivumishi kadhaa kudhihirisha uhamishaji wa mkazo hasa mkazo msingi kwenye silabi zinazounda vivumishi hivyo, mtafiti baada ya kubainisha vivumishi hivyo alionesha kwa baadhi ya vivumishi teule nguvumsikiko kwa viambajengo hapa chini. Aidha, mtafiti alichambua baadhi ya vivumishi kwa kutumia NFM na baadaye alitumia programu ya Praat ili kuthibitisha kile nadharia isemacho.





Mfano Na.5 unaonesha uchanganuzi wa mkazo namna msigano wa nguvumsikiko unavyojitokeza kwenye neno hilo katika umbo lake la ndani. Hapa kwenye tawi hili imebainika kuwa silabi /zu/ ya mwisho kasoro moja ndiyo ina msikiko mkubwa zaidi kuliko nyingine zote zinazounda neno hilo. Matamshi ya kawaida yanaonesha msikiko mkubwa kwenye silabi ya mwisho kasoro moja /zu/ na imeonekana kuwa na gridi mbili. Silabi nyingine zina gridi moja moja. Baada ya uchambuzi wa NFM ni matumizi ya Praat. Tazama kielelezo chini





**Kielelezo 5 : Mkazo katika Silabi za neno "ki'zungu" (matamshi sahihi)**

Kielelezo Na.5 kinaonesha nguvumsikiko ya kivumishi ***kizungu.*** Matokeo ya PRAAT kwenye kivumishi hiki yameonesha kuwa silabi /zu/ ndiyo inaonesha nguvumsikiko kubwa zaidi ambayo katika kilele chake imefikia **42.00**. Ni shahiri dhahiri kuwa silabi hii imeonekana yenye nguvu zaidi kuliko silabi zote zinazounda kivumishi hiki. Aidha, silabi inayofuata ni **/ngu/** ambayo kilele chake kinafikia **18.00.** Mwisho kabisa tunayo **/ki/** ambayo inakadiria kiwango cha desibeli cha **16.00.** Baada ya haya, tulionesha uchambuzi wa NFM kwa matamshi yasiyo sahihi.




Uchanganuzi wa data katika mfano Na.6 unaonesha namna msigano wa nguvumsikiko wa mkazo unavyojibainisha katika neno hilo katika umbo la ndani. Hivyo, silabi ya kwanza /ki/ ndiyo ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine zinazounda neno hilo. Hii ina maana silabi hiyo ndiyo ina gridi tatu kumanisha kuwa

ina nguvu zaidi kuliko nyingine. Baada ya hapo tulionesha matumizi ya Praat ili kuthibitisha matokeo ya NFM. Tazama kielelezo Na.6 hapo chini.




**Kielelezo 6: Mkazo katika Silabi za neno «kizungu» (matamshi yasiyo sahihi)**

Kielelezo Na.6 kinaonesha nguvumsikiko miongoni mwa silabi zilizounda kivumishi ***kizungu.*** Silabi yenye nguvumsikiko kubwa zaidi kuliko nyingine zote imedhihirika kuwa **/ki/** na imefikia kilele cha **39.00.**

Aidha, silabi nyingine zimeonekana hafifu kwenye «praat». Hii ina maana kuwa wajifunzaji Warundi wamehamisha mkazo msingi kutoka silabi ya mwisho kwenda silabi ya kwanza.


**Viunganishi vilivyodhihirisha kuhawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji**

Sehemu hii makala ilizungumzia viunganishi vilivyodhihirika kuhawilisha mkazo kwa wajifunzaji Warundi. Tazama aya zinazofuata.


**Jedwali Na. 4 : Viunganishi vilivyodhihirisha kuhawilisha Mkazo kwa Wajifunzaji**

| No | Viunganishi vilivyohawilisha mkazo | Uwakilishi kifonetiki usio sahihi | Uwakilishi kifonetiki wenye mkazo sahihi |
|---|---|---|---|
| 1 | lakini | /ˈlakini/ | /laˈki:ni/ |
| 2 | kadhalika | /kaˈðalika/ | /kaðaˈlika/ |
| 3 | lazima | /ˈlazima/ | /la:ˈzima/ |
| 4 | labda | /labda/ | /ˈlabda/ |
| 5 | ingawa | /iŋgawa/ | /iˈŋgawa/ |
| 6 | ijapokuwa | /iˈɟapokuwa/ | /iɟapoˈkuwa/ |
| 7 | pengine | /ˈpɛŋginɛ/ | /pɛˈŋginɛ/ |
| 8 | kama | /kama/ | /ˈkama/ |
| 9 | Isitoshe | /isitɔ: ʃɛ/ | /isiˈtɔ: ʃɛ/ |
| 10 | aidha | /ajiða/ | /ˈajiða/ |

Kama jedwali Na.4 linavyobainisha uwezekano wa vivumishi kadhaa kudhihirisha uhamishaji wa mkazo hasa mkazo msingi kwenye silabi zinazounda vivumishi hivyo, mtafiti baada ya kubainisha viunganishi hivyo alionesha kwa baadhi ya viunganish teule nguvumsikiko kwa viambajengo hapa chini. Kwanza alichambua viunganishi hivyo kwa kutumia NFM na baadaye matumizi ya programu ya Praat.





Uchanganuzi wa data katika mfano Na.7 unaonesha namna msigano wa msikiko wa mkazo unavyojibainisha katika neno hilo katika umbo lake landani. Silabi ya mwisho kasoro moja ndiyo ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine zinazounda neno hilo. Silabi hiyo ni /**zi**/ ndiyo ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine katika neno hilo. Kutokana na msigano wa kimsikiko, silabi inayosikika kwa nguvu zaidi zinapewa alama **N** kuonesha kuwa ina nguvu zaidi kimsikiko. Silabi zinazosikika kwa uhafifu zimepewa alama H huonesha kuwa silabi hizo msikika hafifu zaidi. Baada ya hapo ni matumizi ya Praat.





**Kielelezo 7: Mkazo katika Silabi za neno «la'zima» (matamshi sahihi)**

Kielelezo Na.7 kinaonesha nguvumsikiko miongoni mwa silabi zilizounda kiunganishi ***lazima.*** Silabi **/zi/** ndiyo silabi ya mwisho kasoro moja na imeonesha ina nguvumsikiko kubwa zaidi ambayo katika kilele chake kinafikia **38.00** ambayo ni kubwa zaidi kuliko silabi zote katika neno hili. Kisha, inafuata silabi **/ma/** na imeonekana kufikia kiwango cha **25.00.** Mwisho kabisa ni silabi **/la/** ambayo imekadiria kiwango cha desibeli ama kilele cha **23.00.** Baada ya mfano wa matamshi kinadharia, mtafiti alionesha mfano wa matamshi yasiyo sahihi kinadharia kisha matamshi yake kupitia programu ya PRAAT.

`Lazima




Mfano Na.8 unaonesha katika uchanganuzi wa mkazo namna msigano wa nguvumsikiko unavyojitokeza kwenye neno hilo katika umbo lake la ndani. Imebainika kuwa silabi ya kwanza /la/ ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine katika neno hilo. Kutokana na msigano wa kimsikiko silabi inayosikika kwa nguvu zaidi inapewa alama **N** kuonesha kuwa ina nguvu zaidi kimsikiko kuliko silabi zinazobaki. Aidha, silabi nyingine zinakuwa na uhafifu zaidi kuliko ile iliyodhihirika kuwa na nguvu zaidi. Silabi hizo zinapewa alama **H** kuonesha kuwa hazina nguvu. NFM kupitia matawi tunaona kuwa silabi /la/ ndiyo ina gridi nyingi; yaani tatu ilihali nyingine mbili au moja. Hii ina maana wajifunzaji wamehamisha mkazo kutoka silabi ya mwisho kasoro moja kwenda silabi ya kwanza.




**Kielelezo 8 : Mkazo katika Silabi za neno «'lazima» (matamshi yasiyo sahihi)**

Kielelezo Na.8 kinaonesha nguvumsikiko miongoni mwa silabi zinazounda kivumishi **lazima.** Silabi **/la/** ni ya kwanza katika neno hili na inaonesha nguvumsikiko zaidi kuliko silabi zote zinazounda neno hili. Aidha, silabi hii imefikia kilele cha 41.00 ilihali silabi nyingine zimeonekana kama zenye uhafifu zaidi kuliko silabi hiyo ya kwanza. Licha ya silabi hizo kuwa hafifu zinatofautiana kimsikiko. Silabi **/zi/** ya pili kwenye neno hilo imeonekana kuwa na kilele cha **20.00** kisha silabi ya mwisho **/ma/** imeonekana kuwa na kilele cha **16.00.** Hivyo, ni shahiri dhahiri kuwa wajifunzaji Warundi wamehawilisha mkazo kutoka silabi moja kwenda nyingine.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Makala hii ilishughulikia lengo la uhawilishaji mkazo kwa Warundi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili katika vyuo vikuu vya serikali Burundi. Vilevile, makala hii imeweka wazi maneno mbalimbali ambayo huwa yanatatiza wajifunzaji Warundi kutamka mpaka wakahawilisha mkazo kutoka silabi moja hadi nyingine. Baadhi ya maneno hayo yalikuwa ni nomino, viunganishi, vitenzi pamoja na vivumishi. Jambo kama hili linaweka bayana kuwa katika taaluma ya fonolojia, kuliongezwa mchango mkubwa wa kitaaluma hasa kwa watafiti katika uwanja huu wa kimatamshi lakini pia kwa wasomaji vitabu, waandaji mitaala katika kunufaika mengi yanayohusiana na fonolojia na vipengele vyake kwa ujumla. Yaani mwongozo huu ulikuwa haujabainishwa katika uwanja wa fonolojia. Hivyo, utafiti huu umeoneka kichocheo cha tafiti nyingine za baadaye.

**Mapendekezo:** Ni kwa mantiki hiyo makala yetu imetoa mapendekezo kwa tafiti fuatizi kuweza kufanya utafiti kuhusiiana na sababu zinazowapelekea wajifunzaji Warundi wahamishe mkazo kwenye baadhi ya maneno ya Kiswahili, utafiti ufanyike ili kujua kipi kifanyike ili kuondokana na changamoto hizo kwa wajifunzaji husika lakini pia utafiti ufanyike katika vipengele vingine vya isimu tofautina mkazo kama kiimbo, kidatu, lafudhi, n.k.

## MAREJELEO

Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar (Including Intonation)*. Longman Group Ltd.

Crystal, D. (2008). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics* (6th ed.). Basil Blackwell Ltd.

G. (2013). Tons lexicaux et tons intonatifs en frontière intonative en kirundi: Analyse de parole en situation de narration. In *5e Conférence Internationale sur les Langues Bantu*, Paris, June 12–15, 2013.

Halle, M., & Clements, G. N. (1983). *Problem Book in Phonology: A Workbook for Introductory Courses in Linguistics and in Modern Phonology*. MIT Press.
Halle, M., & Vergnaud, J.-R. (1978). *Metrical Structures in Phonology*. MIT Press.
Hogg, R., & McCully, C. B. (1987). *Metrical Phonology: A Coursebook*. Cambridge University Press.
Kindija, R. (2012). *Taaluma Ya Fonetiki Matamshi*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
Liberman, M., & Prince, A. (1977). On stress and linguistic rhythm. *Linguistic Inquiry, 8*(2), 249–336.
Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia Ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari Na Vyuo*. TUKI.
Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi Ya Isimu Na Falsafa Ya Lugha*. TUKI.
Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo Katika Nadharia Ya Fonolojia*. TUKI.
Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi Ya Fonolojia*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
Masuba, S. (2013). *Je, Kinyakyusa Kina Mkazo Au Toni?* (Unpublished master's thesis). University of Dar es Salaam.
Mgullu, S. R. (1999). *Mtaala Wa Isimu*. Longhorn Publishers Ltd.
Mwansoko, H. J. M. (1995). Shadda katika Kiswahili. *Kioo Cha Lugha, 1*(1).
Newmark, P. (1983). *Approaches To Translation*. Pergamon Press.
Polome, E. C. (1976). *Swahili Language Handbook*. Center for Applied Linguistics.
Vital, J. A. (1985). Aspects of Swahili stress. *Kiswahili, 52*(2), 106–113.